



RUZUKU KWA WAANDISHI WA HABARI NA VYOMBO VYA HABARI

Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (**Tanzania Media Fund – TMF**) unawakaribisha waandishi wa habari na taasisi za habari kutuma maombi ya ruzuku. Mwisho wa kutuma maombi kwa ruzuku za mikoani na za upeo mpana ni tarehe 15/ 02/ 2009. Baada ya tarehe hiyo tutaendelea kupokea maombi ya ruzuku za chap chap na za taasisi tu.

TMF NI NINI?

TMF ni Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania, unaokusudia kukuza uhuru na ubora wa vyombo vya habari kwa kujikita zaidi katika habari za maslahi ya umma na uchunguzi. TMF inaamini kuwa vyombo huru vya habari ni roho ya jamii huru na ya kidemokrasia. Ni kwa msingi huu tunatoa ruzuku kwa waandishi wa habari mmoja mmoja na taasisi za kihabari wanaotaka kufuatilia miradi ya habari za maslahi kwa umma na zile za uchunguzi kote nchini Tanzania bara na Zanzibar.

TMF inatoa **ruzuku** kiushindani unaoambatana na **Mpango wa Jifunze** ili kukuza ubora wa habari.

NANI ANAWEZA KUOMBA RUZUKU?

- Chombo cha habari, jumuiya za wanahabari, asasi za kiraia zinazojishughulisha na habari na taasisi za mafunzo ya habari. Taasisi lazima iwe imesajiliwa Tanzania bara au Zanzibar. Aidha iwe hai katika shughuli za kihabari kwa muda usiopungua mwaka mmoja.
- Mwandishi mmoja mmoja anayefanya kazi za kihabari nchini Tanzania au ambaye wasomaji na wasikilizaji wake ni Watanzania. Awe na cheti cha uandishi wa habari au mwenye uzoefu wa habari usiopungua miaka miwili

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Ruzuku za Taasisi

TMF inatumia hatua mbili za maombi kwa taasisi kupunguza kazi isiyokuwa ya lazima kwa mwombaji.

Hatua ya **kwanza** ni kutuma maelezo ya wazo lako katika ukurasa mmoja kwa kutumia fomu maalum. TMF itatathmini maelezo ya wazo kubaini iwapo wazo hilo linakidhi viwango. Wazo likiidhinishwa, utaingia katika hatua ya pili.

Hatua ya **pili** ni kutuma maelezo ya maombi kamili kwa kutumia fomu maalum. Inachukua muda wa wiki 12 kushughulikia maombi ya taasisi tangu tarehe ya mwisho wa kutuma maombi. Tutakujulisha kila hatua ya maombi yako.

Mwombaji anaweza kupata fomu maalum kutoka ofisini kwetu au katika tovuti yetu

<http://www.tmf.or.tz/en/node/25>

Maombi yatumwe yakiwa na nakala pamoja na:

- a) Katiba ya taasisi (constitution)
- b) Hati za usajili wa kampuni (memorandum and articles of association)
- c) Cheti cha usajili (certificate of registration)

Ruzuku za Mwandishi mmoja mmoja

Mwombaji anatuma maelezo ya wazo sambamba na maombi kamili kwa kutumia fomu moja maalum. Fomu zinapatikana kutoka ofisini kwetu au katika tovuti yetu <http://www.tmf.or.tz/en/node/39>. Tunatumia wiki 8 kushughulikia maombi ya mwandishi mmoja mmoja hususan ruzuku za mkoani na upeo mpana tangu tarehe ya mwisho ya kupokea maombi.

Maombi yatumwe yakiwa na nakala pamoja na:

- a) Maelezo binafsi (CV)
- b) Picha moja ndogo (passport-size photo)
- c) Nakala ya kazi zako ulizowahi kuchapa au kurusha hewani kupitia redio au televisheni
- d) Majina mawili na mawasiliano ya watu wanaokufahamu

Maombi yote yatumwe kwa barua pepe, posta au kuletwa moja kwa moja ofisini.

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti yetu

Maombi yatumwe kwa:

Meneja wa Programu
Tanzania Media Fund
S.L.P 38266
1124 Barabara ya Chole
Dar es Salaam
Tanzania

Email: info@tmf.or.tz [tel] +255 22 2601080/2 [fax] +255 22 2601096

TMF haivumilii aina yoyote ya Rushwa.Unaweza kutoa ripoti ya rushwa kwa siri kupitia concern@tmf.or.tz au +255 22 2601080/2